TANGAZO LA SERIKALI Na……..…. la tarehe……..……

_____

KANUNI

_____

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI,
(SURA YA 413)

_____

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 45 (2))

_____

KANUNI ZA LESENI ZA WATOA HUDUMA KWA NJIA YA RELI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA 2024

MPANGILIO WA KANUNI

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Kanuni Jina

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MAOMBI YA LESENI ZA WATOA HUDUMA ZA RELI

4. Zuio kwa watoa huduma wasio na leseni
5. Maombi ya leseni.
6. Sifa za kupata leseni.
7. Ukaguzi.
8. Daftari la leseni.
9. Makundi ya huduma.
10. Aina za leseni.
11. Leseni ya muda mfupi.
12. Leseni ya kawaida.
13. Leseni maalum.
14. Ada za leseni na tozo nyinginezo.

SEHEMU YA TATU
KAMATI YA LESENI

15. Kuanzishwa kwa Kamati ya leseni za reli.
16. Ushirikishaji wa mtaalam wa nje
17. Majukumu ya Kamati.

SEHEMU YA NNE
UTOAJI WA LESENI

18. Utoaji wa leseni.
19. Kukataa kutoa leseni.

20. Taarifa.
21. Notisi ya kufanya marekebisho.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA LESENI

22. Masharti ya leseni.
23. Kutohamisha umiliki wa leseni.
24. Kuhuisha leseni.
25. Ufuatiliaji wa mara kwa mara.

SEHEMU YA SITA
USITISHAJI NA UFUTAJI WA LESENI

26. Usitishaji na ufutaji wa leseni.
27. Notisi ya utetezi.
28. Kurejeshewa leseni.
29. Ukomo wa huduma.
30. Mapitio.

SEHEMU YA SABA
MASHARTI YA JUMLA

31. Makosa na adhabu.

_____
MAJEDWALI
_____

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI,
(SURA YA 413)

_____

KANUNI

_____

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 45 (2))

_____

KANUNI ZA LESENI ZA WATOA HUDUMA KWA NJIA YA RELI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA 2024

SEHEMU YA KWANZA

MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina	1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Leseni za Watoa Huduma kwa Njia ya Reli za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Mwaka 2024.
Matumizi	2. Kanuni hizi zitatumika kwa watoa huduma kwa njia ya reli Tanzania Bara.
Tafsiri	3. Katika Kanuni hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-
Sura ya 413	"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini;
Sura ya 413	"Mamlaka" itakuwa na maana kama ilivyoainishwa katika Sheria;
	"Kamati" maana yake ni Kamati ya Leseni za Reli iliyoanzishwa chini ya kanuni ya 14;
Sura ya 413	"Mkurugenzi Mkuu" itakuwa na maana kama ilivyoainishwa katika Sheria;
	"msimamizi wa miundombinu" maana yake ni Shirika lililoanzishwa kwa lengo la kusimamia miundombinu ya reli;
	"mfumo wa usimamizi wa taarifa" unajumuisha vifaa tumizi na programu tumizi zinazotumika kuhifadhi, kuchakata, kutunza taarifa za usafiri wa reli na kurejesha taarifa zinazohitajika kwa ajili ya kuboresha ufanisi kwa kujiendesha kiotomatiki na kuboresha michakato ya usafiri wa umma ikiwa ni pamoja na kupanga, kukadiria muda wa kusafiri, ucheleweshaji, kurekodi matukio na ajali na ufuatiliaji wa treni;
	"leseni" maana yake ni leseni inayotolewa kwa watoa huduma kwa njia ya reli kwa mujibu wa Kanuni hizi;
Sura ya 413	"Waziri" itakuwa na maana kama ilivyoainishwa katika Sheria;
	"mtoa huduma" maana yake ni mtoa huduma za usafiri wa reli aliyepewa leseni na Mamlaka kwa mujibu wa Kanuni hizi;
	"mfumo wa usimamizi wa usalama" maana yake ni mfumo unaojitosheleza uliosanifiwa kusimamia vipengele vya usalama eneo la kazi;
	"mpango wa usalama" maana yake ni nyaraka iliyoandaliwa na mtoa huduma inayobainisha vipengele katika mfumo wa usimamizi wa usalama;

	"kanuni za uendeshaji wa stesheni" maana yake ni mjumuiko wa masharti na kanuni mahsusi zilizoandaliwa ili kuimarisha uendeshaji salama wa treni katika stesheni husika; na
	"kanuni za jumla za uendeshaji wa treni" maana yake ni masharti ya jumla na mwongozo unaotumika kusimamia uendeshaji wa treni.
SEHEMU YA PILI MAOMBI YA LESENI ZA WATOA HUDUMA ZA RELI	
Zuio kwa watoa huduma wasio na leseni	4. Mtu au shirika hatatoa huduma za usafiri wa reli bila kuwa na leseni halali iliyotolewa na Mamlaka.
Maombi ya leseni	5.- (1) Mtu au shirika linalokusudia kutoa huduma za usafiri wa reli ataomba leseni kwa Mamlaka.
	(2) Maombi ya leseni chini ya Kanuni ndogo ya (1) yataambatishwa na:
	(a) katiba ya kampuni au hati nyingine ya kisheria iliyoanzisha shirika;
	(b) cheti cha usajili;
	(c) ripoti ambayo itajumuisha maelezo ya mawanda ya huduma inayotarajiwa kutolewa;
	(d) mpango wa usalama;
	(e) cheti cha tathmini ya athari ya mazingira;
	(f) taarifa ya hesabu za fedha zilizokaguliwa kwa miaka mitatu iliyopita;
	(g) tozo zinazopendekezwa;
	(h) muundo wa shirika unaojimuisha idadi ya wafanyakazi, uzoefu wa reli na mchanganuo wa vitengo vya taasisi;
	(i) uwezo wa kifedha wa uendeshaji wa biashara ya reli;
	(j) mwongozo wa dereva wa treni;
	(k) taratibu za kawaida za uendeshaji kwenye vituo vikubwa na karakana;
	(l) mwongozo wa matengenezo;
	(m) masharti ya ubebaji;
	(n) wajibu na makatazo kwa abiria;
	(o) utaratibu wa urejeshaji wa fedha inapotokea ucheleweshaji na usitishaji wa safari;
	(p) usimamizi wa malalamiko;
	(q) utaratibu wa kuwahudumia walemavu na wasiojiweza kwenye treni;
	(r) nakala iliyothibitishwa iliyotolewa na msimamizi wa miundombinu; na
	(s) uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi ya leseni.
	(3) Maombi ya leseni ya utoaji wa huduma za reli yatawasilishwa katika fomu iliyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza.
	6. Mtu au shirika atakuwa na sifa za kupata leseni endapo-

Sifa za kupata leseni	(a) limesajiliwa chini ya Sheria ya Kampuni au iliyoanzishwa na sheria nyinginezo;
	(b) lina mkurugenzi au mbia ambaye hajatiwa hatiani kwa kosa lolote linalohusu-
	(i) usalama wa taifa;
	(ii) uhujumu uchumi;
	(iii) udanganyifu, kughushi, rushwa na ufisadi;
	(iv) kutolipa au kukwepa kodi yoyote au ushuru unaolipwa kwa mujibu wa sheria yoyote; na
	(v) utu na maadili;
	(c) hajatangazwa kuwa mufilisi; na
	(d) hajawahi kukiuka kanuni za usalama wa kitaifa na kimataifa katika huduma zinazodhibitiwa.
Ukaguzi	7.-(1) Mamlaka itafanya ukaguzi wa vichwa vya treni, mabehewa na miundombinu kabla ya kutoa leseni na kuandaa taarifa ya ukaguzi.
	(2) Taarifa ya ukaguzi iliyoandaliwa chini ya Kanuni ndogo ya (1) itakuwa msingi wa kukidhi maombi ya leseni.
Daftari la leseni	8.-(1) Mamlaka itatunza na kuweka daftari la leseni zinazotolewa chini ya Kanuni hizi katika nakala mango au nakala tete.
	(2) Daftari la leseni lililoanzishwa chini ya Kanuni ndogo ya (1) litakuwa na nakala zote za leseni zilizoidhinishwa pamoja na nyaraka zinazohusika.
Makundi ya huduma	9. Leseni ya mtoa huduma za reli iliyotolewa na Mamlaka, itakuwa ya kutoa huduma moja au zaidi kati ya zifuatazo:
	(a) huduma za treni ya abiria;
	(b) huduma za treni ya mizigo;
	(c) uendeshaji na ukarabati wa miundombinu ya reli; au
	(d) matengenezo ya vichwa vya treni na mabehewa.
Aina za leseni	10. Mamlaka itatoa aina zifuatazo za leseni kwa watoa huduma-
	(a) leseni ya muda mfupi;
	(b) leseni ya kawaida; au
	(c) leseni maalum.
Leseni ya muda mfupi.	11.-(1) Leseni ya muda mfupi inaweza kutolewa kwa mtoa huduma anayekusudia kutoa huduma za reli kwa muda usiozidi miezi mitatu.
	(2) Leseni ya muda mfupi inaweza kutolewa kwa mtu au shirika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi maalum.
	(3) Maombi ya leseni ya muda mfupi yatakuwa kama ilivyoainishwa katika Fomu B iliyopo katika Jedwali la Pili.
Leseni ya kawaida	12.- (1)Leseni ya kawaida inaweza kutolewa kwa mtoa huduma kwa muda usiozidi miaka kumi na tano.
	(2) Maombi ya leseni ya kawaida yatakuwa kama ilivyoainishwa katika Fomu A iliyopo katika Jedwali la Pili

Leseni Maalum	13. – (1) Leseni maalum inaweza kutolewa kwa mtoa huduma kwa muda zaidi ya miaka kumi na tano.
	(2) Bila kuathiri uwezo wa jumla wa Mamlaka wa kutoa leseni chini ya kanuni hizi, leseni maalum itatolewa baada ya kufanya mashauriano na Waziri.
	(3) Maombi ya leseni maalum yatakuwa kama ilivyoainishwa katika Fomu C iliyopo katika Jedwali la Pili
Ada za leseni na tozo nyinginezo	14.-(1) Mtoa huduma atalipa kwa Mamlaka ada na tozo nyinginezo kwa ajili ya leseni kwa kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Pili.
	(2) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ndogo ya (1), Mamlaka itatoza ada kulingana na makundi na aina za huduma kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.
	(3) Ada na tozo nyinginezo zinazolipwa chini ya Kanuni ndogo ya (1) zitalipwa kwa Mamlaka na kuthibitishwa kwa risiti.
SEHEMU YA TATU KAMATI YA LESENI	
Kuanzishwa kwa Kamati ya leseni za reli	15.-(1) Kutakuwa na Kamati ya leseni za reli itakayoanzishwa na Mkurugenzi Mkuu kwa lengo la kuwezesha ushughulikiaji wa maombi ya leseni.
	(2) Kamati itajumuisha wajumbe wasiopungua watano walioteuliwa na Mkurugenzi Mkuu kutoka katika idara na vitengo vya Mamlaka au sehemu nyingine kama itakavyofaa.
	(3) Kwa kuzingatia Kanuni ndogo (2) Kamati itaundwa na wajumbe wafuatao:
	(a) mkurugenzi wa Udhibiti Reli, ambaye atakuwa mwenyekiti wa Kamati;
	(b) mjumbe mmoja kutoka Kurugenzi ya Udhibiti Reli;
	(c) mjumbe mmoja kutoka Kitengo cha Huduma za Sheria;
	(d) mjumbe mmoja kutoka Kurugenzi ya Udhibiti Uchumi; na
	(e) mjumbe mmoja kutoka Kurugenzi ya Udhibiti Usafiri Barabara.
	(4)Akidi ya kikao cha Kamati itakuwa wajumbe watatu waliohudhuria.
	(5)Maamuzi ya Kamati yatakuwa ya wajumbe wengi.
	(6) Katibu wa Kamati atateuliwa na Mkurugenzi Mkuu kutoka miongoni mwa watumishi wa Mamlaka.
Ushirikishaji wa mtaalam wa nje	16. Bila kujali masharti ya kanuni ya 14, Mkurugenzi Mkuu anaweza kuwashirikisha wataalam wa usafirishaji kutoka nje ya Mamlaka wenye uzoefu usiopungua miaka kumi kuwa sehemu ya Kamati pale anapoona inafaa.
Majukumu ya Kamati	17. Majukumu ya Kamati yatakuwa-
	(a) kuzingatia na kupitia taarifa za ukaguzi wa leseni zilizoandaliwa na Mamlaka;
	(b) kutathmini na kuhakiki uzingatiaji wa maombi, sifa na matakwa ya leseni; na
	(c) kumshauri Mkurugenzi Mkuu juu ya kukidhi sifa za maombi ya leseni.

SEHEMU YA NNE UTOAJI WA LESENI	
Utoaji wa leseni	18. baada ya kupokea maombi ya leseni ya utoaji wa huduma za usafiri wa reli, Mamlaka itayafanyia kazi na endapo ikijiridhisha itatoa leseni.
Kukataa kutoa leseni	19. (1) Mamlaka inaweza kukataa kutoa leseni baada ya kufanya uchambuzi na itamjulisha kwa maandishi muombaji wa leseni sababu za kukataliwa.
	(2) Muombaji ambaye maombi yake yamekataliwa, anaweza kusahihisha dosari na kuwasilisha tena maombi ndani ya siku kumi na nne tangu kupokea taarifa ya kukataliwa kwa maombi yake.
	(3) Muombaji ambaye ameshindwa kuwasilisha tena maombi ndani ya muda ulioainishwa chini ya Kanuni ndogo ya (2) atatakiwa kuwasilisha upya maombi.
Taarifa	20. Mkurugenzi Mkuu atamtaarifu muombaji kuhusu maamuzi ya Mamlaka kwa kutumia anuani iliyopo kwenye fomu ya maombi.
Notisi ya kufanya marekebisho	21.-(1) Endapo Mamlaka itabaini mapungufu yanayosababisha mtoa huduma kutokidhi vigezo vya Sheria au Kanuni hizi, Mamlaka inaweza kutoa notisi ya kufanya masahihisho ili kurekebisha mapungufu ndani ya muda ulioainishwa kwenye notisi.
	(2) Notisi ya kufanya marekebisho inayotolewa chini ya Kanuni ndogo ya (1) itakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne.
SEHEMU YA TANO MASHARTI YA LESENI	
Masharti ya leseni	22.-(1) Kwa kuzingatia Kanuni hizi, mmiliki wa leseni atatakiwa-
	(a) kuhakikisha kuwa, hafanyi mabadiliko ya shughuli au usimamizi bila ridhaa ya maandishi kutoka kwa Mamlaka;
	(b) kufanya matengenezo stahiki ya Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa ili kufuatilia utendaji na maendeleo ya huduma za reli;
	(c) kuhakikisha taarifa zilizotolewa kutoka kwa Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa zinawasilishwa kila mwezi au kwa vipindi vingine vilivyoainishwa na Mamlaka;
	(d) kuhakikisha kuwa, mfumo wa usimamizi taarifa za uhasibu haukinzani na sheria zilizopo;
	(e) kuwasilisha kwa Mamlaka taarifa za hesabu zilizokaguliwa ndani ya miezi mitatu baada ya kuisha kwa kila mwaka wa fedha; na
	(f) kuwa na bima kwa huduma anazotoa kulingana na mkataba alioingia baina yake na msimamizi wa miundombinu.
	(2) Mmiliki wa leseni ataanzisha na kuzingatia-
	(a) sera na mpango wa usalama;

	(b) mfumo sahihi wa tiketi;
	(c) kanuni za jumla za uendeshaji treni;
	(d) kanuni za uendeshaji wa stesheni;
	(e) mwongozo wa uendeshaji wa madereva na wafanyakazi wa treni; na
	(f) mfumo wa usimamizi wa usalama.
	(3) mmiliki wa leseni ataandaa utaratibu wa-
	(a) kuzingatia masharti ya viwango vya huduma bora;
	(b) utaratibu wa namna ya kuwahudumia walemavu na wasiojiweza; na
	(c) utaratibu wa kushughulikia malalamiko.
	(4) Mmiliki wa leseni atazingatia masharti yaliyomo katika Cheti cha Tathmini ya Athari za Mazingira
	(5) Mmiliki wa leseni atalipa kwa wakati ada na ushuru kwa Mamlaka.
	(6) Mmiliki wa leseni ataitaarifu Mamlaka na kuwasilisha leseni kwa ajili ya mapitio endapo -
	(a) kuna mabadiliko katika mawanda na namna ya uendeshaji;
	(b) mabadiliko katika umiliki wa hisa; au
	(c) mabadiliko ya mkataba baina yake na msimamizi wa miundombinu.
	(7) Mmiliki wa leseni ataruhusu kufanyika kwa huduma za dharura kama itakavyoelekezwa na Mamlaka.
	(8). Mmiliki wa leseni atahakikisha anafanya kazi kwa kuzingatia mwenendo mzuri, weledi wa kitaaluma na tija ya kifedha wakati wote.
	(9). Mmiliki wa leseni ataajiri madereva na wafanyakazi wa treni ambao wamethibitishwa na kusajiliwa na Mamlaka.
Kutohamisha umiliki wa leseni	23. Leseni iliyotolewa chini ya Kanuni hizi haitahamishwa umiliki bila idhini ya Mamlaka.
Kuhuisha leseni	24.-(1) Mmiliki wa leseni anayetaka kuhuisha leseni ataomba kwa Mamlaka ndani ya siku thelathini kabla ya tarehe ya kuisha kwa muda wa leseni.
	(2) Mamlaka inaweza kutoza asilimia hamsini zaidi ya ada ya leseni kwa maombi yaliyowasilishwa siku kumi na nne baada ya kumalizika muda wa leseni na riba ya asilimia tano ya kiasi kilicholimbikizwa kila baada ya siku thelathini kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili.
	(3) Mamlaka haitazingatia maombi ya kuhuisha leseni kwa mtoa huduma ambaye ana malimbikizo ya adhabu kwa maombi yaliyowasilishwa.
Ufuatiliaji wa mara kwa mara	25.-(1) Ili kuhakikisha uzingatiaji wa masharti ya leseni, Mamlaka itafanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwenye majengo na miundombinu ya mtoa huduma.
	(2) Mamlaka inaweza, wakati wa kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara-
	(a) kuingia, kukagua na kuhakiki vichwa vya treni, mabehewa na miundombinu ya reli;

	(b) kufanya mahojiano na kuchukua maelezo ya maandishi kutoka kwa mfanyakazi yeyote;
	(c) kuhakiki na kufanya uchunguzi kuhusu hali ya kazi yoyote, vichwa vya treni na mabehewa au vitu vingine vilivyotumika kwa au vinavyokusudiwa kutumika kwa au kuhusiana na usafirishaji wa abiria au mizigo kwa njia ya reli; na
	(d) kutoa notisi ya maandishi inayoelekezwa kwa mtoa huduma kumtaka ajibu au kutoa taarifa ya hoja zilizoibuliwa naye endapo anaona umuhimu wa kufanya hivyo.
SEHEMU YA SITA USITISHAJI NA UFUTAJI WA LESENI	
Usitishaji na ufutaji wa leseni	26.-(1) Mamlaka inaweza kusitisha au kufuta leseni iwapo-
	(a) mtoa huduma atashindwa kutoa huduma iliyokusudiwa ndani ya miezi sita tangu tarehe ya kuanza kutumika kwa leseni;
	(b) kibali cha mtoa huduma kimefutwa na msimamizi wa miundombinu;
	(c) mtoa huduma atatoa taarifa ya udanganyifu kwenye maombi ya leseni; na
	(d) mtoa huduma atashindwa kuzingatia notisi ya marekebisho iliyotolewa chini ya Kanuni ya 21 ya Kanuni hizi.
	(2) Mamlaka inaweza kumuagiza mtoa huduma kufanya marekebisho ya mapungufu ya uendeshaji au masharti yoyote ya leseni ambayo kwa maoni yake yamekiukwa.
Notisi ya utetezi	27.-(1) Endapo mtoa huduma anashindwa kufuata masharti ya Kanuni ya 22, Mamlaka inaweza kutoa notisi ya kumtaka mtoa huduma kuwasilisha utetezi juu ya sababu za kutositishwa au kutofutwa kwa leseni ndani ya siku ishirini na moja tangu tarehe ya notisi.
	(2) Endapo mtoa huduma anashindwa kujibu ndani ya muda ulioainishwa katika Kanuni ndogo ya (1) au Mamlaka haijaridhishwa na sababu zilizotolewa na mtoa huduma, Mamlaka inaweza kusitisha au kufuta leseni ndani ya siku ishirini na nane.
Kurejeshewa leseni	28. Ikitokea leseni imesitishwa, Mamlaka inaweza kurejesha leseni baada ya kutimiza masharti kama yalivyoainishwa kwenye notisi ya usitishwaji.
Ukomo wa huduma	29.- Endapo leseni iliyotolewa chini ya Kanuni hizi imesitishwa au imefutwa, mtoa huduma ataacha kutoa huduma.
Mapitio TS Na. 73 la 2020	30. Mtu ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa Mamlaka chini ya Kanuni hizi anaweza, ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya uamuzi huo, kutuma maombi kwa Mamlaka kwa ajili ya mapitio kwa utaratibu ulioainishwa na Kanuni za Mapitio za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini.
SEHEMU YA SABA MASHARTI YA JUMLA	

Makosa na adhabu	31. Mtu atakayekiuka au kushindwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni tatu au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5 (3))

FOMU YA MAOMBI YA LESENI YA MTOA HUDUMA ZA RELI

SEHEMU A: TAARIFA ZA MWOMBAJI

Jina la Kampuni: ……

Namba ya Cheti cha Usajili/Namba ya Usajili:……..……

Tarehe ya kutolewa: ……

Mahali biashara iliposajiliwa: ……..

Anwani: ……

Sanduku la Posta: ……..

Namba ya simu: ……..

Barua pepe: ……

Namba ya kibali: ……..

Jedwali la Taarifa za Umiliki wa Hisa:

Na.	**Jina**	**Uraia**	**Anwani**	**Asilimia za hisa**

SEHEMU B: AINA NA MAKUNDI YA LESENI

i. Aina za leseni

Na.	**Aina ya leseni iliyotolewa**	**Chagua inayofaa**
1.	Leseni ya kawaida	
2.	Leseni ya muda mfupi	
3.	Leseni maalum	

ii. Makundi ya huduma

SN	Makundi ya huduma inayotolewa	Chagua inayofaa
1.	Huduma za treni ya abiria	
2.	Huduma za treni ya mizigo,	
3.	Uendeshaji na ukarabati wa miundombinu ya reli	
4.	Matengenezo ya vichwa vya treni na mabehewa	

Maelezo mafupi na mawanda ya huduma itakayotolewa:

……
……
……
……
……

SEHEMU C: AINA YA MAOMBI *Maombi mapya* ☐ *kuhuisha* ☐

Taarifa ya leseni iliyoisha (kama ipo)

Namba ya leseni: …….. Tarehe ya kuisha……

Taarifa ya jumla, ikiwemo kumbukumbu juu ya rasilimali fedha za Mwombaji (Ambatanisha kurasa za ziada ikiwa ni lazima).

……
……
……
……

SEHEMU D: TAMKO

Mimi …… natamka kwamba maelezo yaliyotolewa katika maombi haya ni ya kweli, sahihi na kamili kwa kadri ya ufahamu wangu. Ninaelewa kwamba kutoa taarifa zozote za uongo kunaweza kusababisha kukataliwa kwa ombi hili au kubatilishwa kwa leseni.

Jina Kamili: ……...…

Cheo: ……

Sahihi: ……...…

Muhuri: ……...

Tarehe: ……

Kiambatisho: ORODHA YA NYARAKA ZA KUWASILISHA

NA.	NYARAKA ZINAZOHITAJIKA	IMEWASILISHWA	HAIJA WASILISHWA
1.	Katiba ya kampuni au hati nyingine ya kisheria iliyoanzisha shirika;		
2.	Cheti cha usajili;		
3.	Ripoti ambayo itajumuisha maelezo ya mawanda ya huduma inayotarajiwa kutolewa;		
4.	Mpango wa usalama;		
5.	Cheti cha tathmini ya athari ya mazingira;		
6.	Taarifa ya hesabu za fedha zilizokaguliwa kwa miaka mitatu iliyopita;		
7.	Tozo zinazopendekezwa;		
8.	Muundo wa shirika ukijumuisha idadi ya wafanyakazi, uzoefu wa reli na mchanganuo wa vitengo vya taasisi;		
9.	Uwezo wa kifedha wa uendeshaji wa biashara ya reli;		
10.	Mwongozo wa dereva wa treni;		
11.	Taratibu za kawaida za uendeshaji kwenye vituo vikubwa na karakana;		
12.	Mwongozo wa matengenezo;		
13.	Masharti ya ubebaji;		
14.	Wajibu na makatazo kwa abiria;		
15.	Utaratibu wa urejeshaji wa fedha inapotokea ucheleweshaji na usitishaji wa safari;		
16.	Usimamizi wa malalamiko;		
17.	Utaratibu wa kuwahudumia walemavu na wasiojiweza kwenye treni;		
18.	Nakala iliyothibitishwa iliyotolewa na msimamizi wa miundombinu; na		
19.	Uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi ya leseni kwa Mamlaka.		

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 13)

ADA ZA LESENI

FOMU A: ADA ZA LESENI YA KAWAIDA.

NA	MAKUNDI YA HUDUMA	ADA YA LESENI YA MWAKA	ADA YA MAOMBI
1.	HUDUMA ZA ABIRIA	US$30,000	US$5,000
2.	HUDUMA ZA MIZIGO	US$40,000	US$7,000
3.	UENDESHAJI NA UKARABATI WA MIUNDOMBINU	US$20,000	US$4,000
4.	MATENGENEZO YA VICHWA VYA TRENI NA MABEHEWA	US$15,000	US$3,000

FOMU B: ADA ZA LESENI YA MUDA MFUPI

NA	MAKUNDI YA HUDUMA	ADA YA LESENI YA MWAKA	ADA YA MAOMBI
1.	HUDUMA ZA ABIRIA	US$6,000	US$1500
2.	HUDUMA ZA MIZIGO	US$8,000	US$1000
3.	UENDESHAJI NA UKARABATI WA MIUNDOMBINU	US$4,000	US$1000
4.	MATENGENEZO YA VICHWA VYA TRENI NA MABEHEWA	US$3,000	US$1000

FOMU C: ADA ZA LESENI MAALUM

NA	MAKUNDI YA HUDUMA	ADA YA LESENI YA MWAKA	ADA YA MAOMBI
1.	HUDUMA ZA ABIRIA	US$60,000	US$5,000
2.	HUDUMA ZA MIZIGO	US$80,000	US$7,000
3.	UENDESHAJI NA UKARABATI WA MIUNDOMBINU	US$40,000	US$4,000
4.	MATENGENEZO YA VICHWA VYA TRENI NA MABEHEWA	US$30,000	US$3,000

JEDWALI LA TATU

(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 22(2))

NOTISI YA MAREKEBISHO

Kwa: ….....

Ninakupa notisi kwa mujibu wa Kanuni ya 22(2), kwamba baada ya siku ……..kuanzia tarehe ya kupokelewa notisi hii, ninakusudia…….(eleza hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa kupunguza hatari) isipokuwa,kabla ya kuisha kwa muda uliowekwa, utetetezi wa kuniridhisha uwe umetolewa kuonesha hatua ulizochukua kurekebisha usalama wa reli au hatua nyingine yoyote iliyochukuliwa kurekebisha mapungufu.

Maeneo yanayohitaji marekebisho ni:

1) ….....
2) ….....
3) ….....
4) ….....
5) ….....

Imetolewa ……..……. **tarehe**…..... **mwezi** …..... **20**……...
Sahihi.....
Jina la Mkaguzi......

Dodoma,
……., 2024

MAKAME MNYAA MBARAWA
Waziri wa Uchukuzi